



Familia Pendwa,

Kurasa zifuatazo zinakuonyesha jinsi ya kufafanua Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi, ambayo inatoa muhtasari wa matokeo ya mwanafunzi wako ya mtihani wa hivi karibuni zaidi wa Utathmini wa Maendeleo ya Mwanafunzi wa Jimbo Lote la Iowa (ISASP, Iowa Statewide Assessment of Student Progress). Mtihani wa ISASP umekusudiwa kutoa maelezo kwa shule na familia kuhusu jinsi wanafunzi wanavyoendelea kulingana na Viwango Vikuu vya Elimu vya Jimbo la Iowa.

Ukurasa wa 1 wa ripoti unaonyesha muhtasari wa jinsi mwanafunzi alivyofanya kwa jaribio la kila somo la ISASP. Kuna alama ya kipimo ya jaribio la somo, picha ya matokeo ya alama ya kipimo na kiwango cha mafanikio kulingana na alama ya kipimo. Ufafanuzi wa matokeo ya mwanafunzi wako unatoa maelezo zaidi kuhusu maarifa na ujuzi wa mwanafunzi wa kawaida katika kiwango cha mafanikio cha mwanafunzi wako.

Ukurasa wa 2 wa ripoti unaonyesha matokeo ya mwanafunzi kwa Vitengo Vikuu vya Elimu vya Jimbo la Iowa vinavyohusishwa na kila jaribio la somo. Vitengo ni sehemu mahususi za maudhui za kuangaziwa kwa somo. Vitengo vimeorodheshwa kwa kila jaribio la somo, na viwango vya matokeo vinaonyesha jinsi mwanafunzi wako alivyofanya ikilinganishwa na matokeo ya wenzake walio katika darasa moja naye katika Jimbo la Iowa.

Ukurasa wa 3 wa ripoti unaonyesha jinsi mwanafunzi wako alivyotenda kwenye mtihani wa sasa wa ISASP ikilinganishwa na alama ambazo mwanafunzi wako alipata katika miaka iliyopita. Grafu hii inathibitisha uchunguzi kuhusu maendeleo ya mwanafunzi wako jinsi inavyoonyeshwa kwenye mabadiliko ya alama baada ya muda.

Ukurasa wa 4 unaonyesha jinsi mwanafunzi wako alivyotenda kwa jaribio la kuandika. Alama ambazo mwanafunzi wako alipata katika sehemu nne (Insha ya Vidokezo, Ubunifu, Mpangilio na Matumizi ya Lugha) zimeonyeshwa, pamoja na alama za wastani za wilaya ya shule yako. Pia, matokeo ya mtihani yameonyeshwa kwenye utaratibu wa Kina cha Maarifa (DOK). Kila kipengele cha mtihani kimehusishwa na DOK inayoonyesha aina na kiwango cha kufikiria na kuelewa mambo ambacho mwanafunzi anahitaji. Sehemu inayoonyesha alama ambazo mwanafunzi wako alipata kati ya alama za jumla zinazotarajiwa katika kila kiwango cha DOK imeonyeshwa.

Unapokagua matokeo ya ISASP, chukua muda wa kuzungumza kuhusu matokeo pamoja na mwanafunzi wako. Uliza maswali na upate maoni kutoka kwa mwanafunzi wako kuhusu sehemu za masomo anazofanya vizuri zaidi, msaada wa ziada utakaomsaidia, na kinachomvutia mwanafunzi wako darasani. Wasiliana na shule yako kuhusu maoni haya na matokeo ya ISASP ili upate maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuendelea kumsaidia mwanafunzi kupiga hatua.

Wako mwaminifu, Mipango ya Mitihani ya Iowa



# ISASP

## IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS

Mtihani wa ISASP ni mtihani mpya wa jimbo lote unaolingana na Viwango Vikuu vya Elimu vya jimbo la Iowa. Unatoa utathmini wa wazi na sahihi wa matokeo ya masomo ya mwanafunzi ambayo yanafaa na yanayoweza kuchukuliwa hatua kwa ajili ya wanafunzi, wazazi, walimu na jimbo. Mwongozo huu unafafanua jinsi ya kusoma **Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi**.

### Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi

#### Ukurasa wa 1 kati ya 4

**1** STUDENT REPORT FIRSTNAME LASTNAME-MATH-NA  
STATE ID# 0123456789  
SCHOOL NAME (5678)  
DISTRICT NAME (1234)

ISASP IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS  
SPRING 2023 GRADE 8

The State of Iowa is committed to delivering a high quality assessment for its students. The Iowa Statewide Assessment of Student Progress (ISASP) is aligned with the Iowa Core Academic Standards.

These results will provide educators, parents, and students important information about student performance that can be used to guide learning to best help each student. More information about your student's achievement level scores can be found at <https://iowa.pearsonaccess.com/performance-levels/>.

To access interpretive information, visit the Information for Families page on the ISASP Portal at <https://iowa.pearsonaccess.com/families/>, or use the Quick Response Code (QR Code) to the right with a smartphone, tablet, or other device.

**2** **3** **4** **5**

**ENGLISH LANGUAGE ARTS TOTAL** Scale Score: **544** Achievement Level: **PROFICIENT**

The English Language Arts (ELA) scale score is the combination of your Reading (999) and Language/Writing (999) scale scores.

A student at this level has the knowledge, skills and abilities to be proficient in ELA. This may include the ability to read, comprehend and analyze literary and informational texts. This may also include the ability to write coherent pieces that are appropriate, organized, and use standard English.

**MATHEMATICS** **No Score Available**

No Mathematics score available. Please see your school for more information.

**SCIENCE** Scale Score: **637** Achievement Level: **ADVANCED**

A student at this level has the knowledge, skills and abilities to be advanced in Science. This includes using the Science and Engineering Practices and Cross-Cutting Concepts and demonstrating an analytical understanding of life, physical, and earth and space science. The student communicates core ideas and concepts using complex practices of science.

<https://iowa.pearsonaccess.com/>  
Page 1 of 4 mmddy-20000000-12345678-0000000

#### 1. MAELEZO YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi, Kitambulisho cha Mwanafunzi cha jimbo la Iowa, shule, wilaya, na darasa huonyeshwa katika sehemu ya juu ya ukurasa wa kwanza.

#### 2. KIPIMO CHA MATOKEO

Kipimo cha Matokeo hutoa picha ya Kiwango cha Mafanikio ya Mwanafunzi. Viwango vya alama kwa kila kiwango cha mafanikio vinaonyeshwa chini ya picha.

#### 3. KIPIMO CHA ALAMA

Kipimo cha Alama ni alama inayoruhusu ulinganishaji wa alama katika madarasa na miaka.

#### 4. KIWANGO CHA MAFANIKIO

Kiwango cha Mafanikio kinaonyesha matokeo ya mwanafunzi kwa mtihani na kutoa maelezo ya jumla kuhusu kitu ambacho mwanafunzi anajua na anaweza kufanya.

#### 5. MAELEZO YA MATOKEO

Maelezo ya Matokeo ni maelezo ya kiwango cha mwanafunzi kuelewa maudhui mahususi kwa kiwango cha darasa.

\*Kumbuka: Ikiwa huoni alama za mtihani **ulioorodheshwa**, tafadhali wasiliana na shule ya mwanafunzi wako kwa maelezo zaidi. Maelezo zaidi kuhusu mtihani wa ISASP na Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi yanapatikana katika <https://iowa.pearsonaccess.com/>



### Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi

### Ukurasa wa 2 kati ya 4

ISASP SPRING 2023	GRADE 8	FIRSTNAME LASTNAME-MATH-NA STATE ID# 0123456789
<b>STUDENT PERFORMANCE BY DOMAIN</b>		
Domain performance can provide insight into your student's strengths and opportunities for improvement. In the tables below your student's performance is displayed by domain.		
<b>ELA-READING Domains</b>	6	STUDENT PERFORMANCE
Key Ideas and Details		Low Middle High
Craft and Structure		✓
Integration of Knowledge and Ideas		✓
<b>ELA-LANGUAGE/Writing Domains</b>		STUDENT PERFORMANCE
Research to Build and Present Knowledge		Low Middle High
Production and Distribution of Writing		✓
Text Types and Purposes		
Conventions of Standard English / Knowledge of Language		✓
Vocabulary Acquisition and Use		✓
<b>MATHEMATICS Domains</b>		STUDENT PERFORMANCE
Functions		Not Available
The Number System		
Expressions and Equations		
Statistics and Probability	7	
Geometry		
<b>SCIENCE Domains</b>		STUDENT PERFORMANCE
Life Science		Insufficient Information
Physical Science		
Earth and Space Sciences		
<a href="https://iowa.pearsonaccess.com/">https://iowa.pearsonaccess.com/</a>		
Page 2 of 4		

#### 6. VITENGO VIKUU VYA ELIMU VYA JIMBO LA IOWA

Vitengo Vikuu vya Elimu vya jimbo la Iowa ni sehemu mahususi za darasa na maudhui za kuangaziwa ambazo hujaribiwa. Kwa mfano, Mawazo *Muhimu na Maelezo* ni kitengo katika mthani wa Kusoma wa darasa la 8.

#### 7. MATOKEO YA KITENGO

Matokeo ya mwanafunzi katika Vitengo Vikuu vya Elimu vya jimbo la Iowa hubainishwa kama Chini, Wastani, au Juu. Katika alama za wanafunzi wote kwenye kila Kitengo, 20% za juu zaidi hubainishwa kama Juu, 20% za chini zaidi hubainishwa kama Chini, na 60% za wastani hubainishwa kama Wastani.

#### MTIHANI WA ISASP HUTATHMINI:

##### *Kusoma*

Kwa Madarasa ya 3 hadi 11

##### *Lugha na Kuandika*

Kwa Madarasa ya 3 hadi 11

##### *Hisabati*

Kwa Madarasa ya 3 hadi 11

##### *Sayansi*

Kwa Madarasa ya 5, 8, na 10



### Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi


### Ukurasa wa 3 kati ya 4

ISASP SPRING 2023 GRADE 8 FIRSTNAME LASTNAME-MATH-NA STATE ID# 0123456789


#### GROWTH

Growth is determined by comparing a student's scale score from a previous year with this year's scale score. The bar graph below displays the range of scale scores associated with each achievement level for the grades in which the ISASP is administered. Your student's scale scores are marked on the corresponding bar graph with a \* (star).


#### ENGLISH LANGUAGE ARTS



#### MATHEMATICS



#### SCIENCE



ACHIEVEMENT LEVELS: NOT YET PROFICIENT PROFICIENT ADVANCED

<https://iowa.pearsonaccess.com/>

Page 3 of 4

### 8. UKUAJI

Ukurasa wa Ukuaji unatoa maelezo kuhusu alama za sasa za mwanafunzi na alama zozote zinazohusishwa na mitihani ya awali ya ISASP.

Pau za rangi zinaonyesha viwango vitatu vya mafanikio, na alama za kipimo za mwanafunzi wako zimeonyeshwa kwenye grafu ya pau na alama ya \*(nyota).

Alama za kipimo kwenye kila sehemu ya somo ziko kwa kipimo cha kawaida na zinaweza kulinganishwa moja kwa moja ili kubainisha jinsi matokeo ya mwanafunzi yalivyobadilika baada ya muda.



### Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi

### Ukurasa wa 4 kati ya 4

ISASP FIRSTNAME LASTNAME-MATH-NA  
 SPRING 2023 GRADE 8 STATE ID# 0123456789

**WRITING RUBRIC SCORES**

Your student's essay was scored on four independent elements of writing: Prompt Task, Development, Organization, and Language Use. Specific descriptions of each score point associated with each element may be found online (<https://iowa.pearsonaccess.com/rubrics/>). The graph shows the scores your student earned on each element. The + (plus) indicates the district Average Score for each element.

Student's Element Scores

Element	Score
Prompt Task	2 of 5
Development	5 of 5
Organization	1 of 5
Language Use	3 of 5

**DEPTH OF KNOWLEDGE (DOK)**

Each item on the ISASP is identified with a depth of knowledge (DOK) level. DOK, or cognitive complexity, reflects the type and level of thinking and reasoning required of students when interacting with a particular item. The table displays a fraction indicating the points your student earned out of the total points possible in that DOK level.

Student's Points Earned / Total Points Possible

	ELA- READING	ELA - LANGUAGE/ WRITING	MATHEMATICS	SCIENCE
Essential Competencies (DOK 1)	7 / 10	6 / 18	No Score Available	Insufficient Information
Conceptual Understanding (DOK 2)	10 / 17	5 / 11	No Score Available	Insufficient Information
Extended Reasoning (DOK 3)	4 / 7	3 / 10	No Score Available	Insufficient Information

<https://iowa.pearsonaccess.com/>  
 Page 4 of 4

### 9. UTARATIBU WA KUANDIKA

Insha za mwanafunzi hupewa alama kulingana na vipengele vinne tofauti vya uandishi:

- Insha ya Vidokezo
- Ubunifu
- Mpangilio
- Matumizi yaLugha

Grafu inaonyesha alama ambazo mwanafunzi wako alipata kwa kila kipengele. Alama ya + (kujumlisha) inaonyesha Alama ya Wastani ya wilaya kwa kila kipengele.

Alama za mwanafunzi wako, na jinsi zinavyolingana na alama za wastani za wilaya, inaweza kuonyesha sehemu anazofanya vizuri zaidi na sehemu anazohitaji kuboresha.

### 10. KINA CHA MAARIFA

Kina cha Maarifa (DOK) huonyesha aina na kiwango cha kufikiria na kufahamu mambo ambacho wanafunzi wanahitaji ili kujibu swali la mtihani (DOK 3 inaonyesha kiwango cha juu cha maarifa ya utambuzi kuliko DOK 1).

Jedwali linaonyesha sehemu zinazoonyesha alama ambazo mwanafunzi wako alipata kati ya alama za jumla zinazotarajiwa katika kiwango cha DOK.

Mtihani wa ISASP huwapa maelezo wanafunzi, wazazi, waalimu na jimbo kuhusu jinsi wanafunzi katika jimbo la Iowa wanavyoendelea kulingana na Viwango Vikuu vya Elimu vya jimbo la Iowa. Unakusudiwa kutoa maelezo muhimu kuhusu sehemu ambazo wanafunzi wanafanya vizuri na sehemu ambazo wanaweza kuhitaji usaidizi wa ziada. Wanafunzi na wazazi wanahimizwa kukagua matokeo ya Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi na kuwasiliana na shule zao kwa maoni zaidi.